# Imagine Math

## Helping your student succeed at school and at home

Mzazi au Mlezi mpendwa,

Karibu! Mwanafunzi wako ameandikishwa katika Imagine Math kwa mwaka mpya wa masomo! Imagine Math ni mpango ingiliani wa hesabu ambao humfunza mwanafunzi wako stadi za hesabu katika kiwango cha ustadi cha mwanafunzi wako na humsaidia kujifunza alichokisoma. Ili kujifunza zaidi kuhusu Imagine Math, tembelea www.imaginelearning.com/math.

### Uzoefu wa Mwanafunzi wako ni Imagine Math

Imagine Math Hutumia mtalaa wastani ili kufunza na kusisitiza stadi za hesabu kuanzia hesabu hadi Jiometri.

**Imagine Math PreK-2** imeundwa kwa wanafunzi wachanga na hulenga stadi za mapema za hesabu kama vile kuhesabu, nambari na matumizi, na ufahamu wa kimantiki. Wanafunzi wachanga huwekwa katika mazingira ya vitabu vya hadithi vyenye wahusika wa kuvutia ambao huwashirikisha wanafunzi na kuonyesha jinsi hesabu inavyopatikana duniani kote. Mwanafunzi wako anapokuwa akicheza katika Imagine Math PreK-2, anaweza kutembelea maeneo tofauti kama vile nyumba ya mti, uwanja wa kuchezea, msitu, au ghala ili kucheza masomo ya hesabu na kutatua hesabu.

**Imagine Math Grade 3+** hulenga stadi za hesabu kwa wanafunzi katika Gredi ya 3-8, Aljebra 1, na Jiometri na masomo ya kawaida ya dhana. Ikiwa mwanafunzi wako anahitaji msaada wa ziada, anaweza kusogoa kwa matini na mwalimu wa hesabu aliyethibitishwa na jimbo na kuona hesabu kwenye skrini. Mwanafunzi wako anapokamilisha masomo ya hesabu, anapata alama ambazo anaweza kutumia kuchangia mashindano ya darasani, kuchangia mashirika ya ufadhili ya ndani ya kitaifa, au kununua viboreshaji vya uhuisho wake.

### Kutumia Imagine Math Nyumbani

Mwanafunzi wako anaweza kufikia Imagine Math katika kivinjari wavuti kutoka kwa kompyuta au kompyuta kibao chochote (hakuna simu mahiri) kwa kuingia kwa kutumia URL na maelezo ya kuingia hapa chini. Angalia help.imaginelearning.com ili kuhakikisha kwamba kompyuta au kompyuta kibao chako kinatimiza mahitaji ya chini ya kiufundi. Ili kudumisha njiailiyobinafsishwa ya kusoma ya mwanafunzi wako na kuripoti ukuaji na maendeleo sahihi, wanafunzi walioandikishwa tu katika Imagine Math ndio wanaopaswa kuitumia nyumbani.

### Kuunga mkono Maendeleo ya Mwanafunzi Wako

Unaweza kumsaidia mwanagunzi wako kufanikiwa kwa kushiriki katika uzoefu wao wa Imagine Math. Fuata mapendekezo haya ili upate mengi kutoka kwa Imagine Math katika mwaka huu wa masomo:

- **Himiza mwanafunzi wako Imagine Math nyumbani.** Hutoa sehemu ya kufanya kazi isiokengeusha fikira na humruhusu mwanafunzi wako kufanya kazi peke yake ili kusuluhisha hesabu.
- **Endelea kushiriki katika uzoefe wa Imagine Math wa mwanafunzi wako.** Muulize ni shughuli na masomo gani aliyokamilisha au ni mashindano au mashirika gani ya ufadhili anayochangia alama zake.
- **Pitia maendeleo ya mwanafunzi wako na mwalimu wake.** Jadili maendeleo ya jumla ya mwanafunzi wako, matokeo ya mtihani, ukuaji kuwadia viwango vya jimbo na kitaifa, na maeneo ya stadi ambapo mwanafunzi wako anaweza kuwa anasumbuka.

---

IMAGINE MATH LOGIN

Student: ______________________________

URL: ______________________________

Username: ______________________________

Password: ______________________________

